BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Tatu – Tarehe 13 Disemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti bora ndani yake.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na Kuweka Masharti bora ndani yake.

## II. MASWALI

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

73. MHESHIMIWA SALHA MOHAMED MWINJUMA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kumekuwa na utaratibu wa mtu anapopata ajali lazima aende kituo cha Polisi kufuata PF3 ili aweze kupatiwa huduma ya matibabu katika hospitali zetu hapa Zanzibar.

(a) Je, ni utaratibu upi unatakiwa kufuatwa ili mwananchi

aweze kupata PF3 katika vituo vya Polisi pindi anapokutwa na ajali.

(b) Je, ni muda gani mtu anatakiwa kupatiwa huduma hiyo ya PF3 baada ya kupata ajali.

(c) Je, Serikali haioni kwamba utaratibu wa kupata PF3 unachangia kuongezeka kwa vifo katika hospitali zetu.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

138. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Hivi karibuni kumetokezea athari za mabadiliko ya tabia Nchi, jambo linalopelekea kuleta maafa na majanga mbali mbali ikiwa ni pamoja na baadhi ya maeneo kuripotiwa kuingia maji ya bahari kwenye makaazi ya watu.

Je, Wizara yako inachukua hatua gani za dharura na zile za muda mrefu katika kukabiliana na tatizo hili.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

109. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuanzisha na kuhamasisha matumizi ya mfumo unaosimamia uuzaji na ununuzi wa bidhaa kwa kutumia risiti za kielektroniki.

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali imefanikiwa tangu mfumo huo uanze kutumika.

(b) Je, kuna changamoto gani inazoikabili Serikali katika utekelezaji wa mfumo huo.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

13. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Naipongeza Wizara yako kwa juhudi kubwa inazozichukua katika kuwasaidia wananchi wetu kupitia suala zima la ujasiriamali, kwa lengo la kuweza kujitegemea baada ya kuwawezesha kiuchumi.

Je, ni kwa kiasi gani suala la elimu ya ujasiriamali limepewa mazingatio katika Wizara yako.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

4. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na juhudi za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhimiza usafi nchini na kuzitaka Halmashauri zetu na Mabaraza ya Miji ya Zanzibar pamoja na viongozi wote na wananchi kwa ujumla kuhamasisha na kusimamia usafi katika maeneo yao, changamoto ya kuzagaa kwa uchafu na muamko mdogo wa kufanya usafi katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar, imeendelea kuiathiri nchi yetu.

(a) Je, Serikali imefanya tathmini ya kuimarika kwa usafi katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar hasa katika maeneo ya mjini.

(b) Je, Serikali inachukua juhudi zipi kuhakikisha Jiji la Zanzibar linakuwa safi.

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya wote wanaoshindwa kuimarisha usafi katika maeneo yao.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

99. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika kujenga Ofisi mpya za Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi zilizopo Kisauni, Unguja, Serikali ilifanya ujenzi wa sehemu ya kusalia. Hata hivyo kumekuwa na manung'uniko na masimango kutoka kwa watumiaji wa sehemu hiyo ya kusalia kutokana na ukweli kwamba, mkandarasi wa ujenzi huo hadi leo hakulipwa pesa zake na Serikali.

(a) Je, ujenzi wa sehemu hiyo ya kusalia uligharimu kiasi gani kama gharama ya ukandarasi na ushauri elekezi.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimelipwa na kiasi gani hakijalipwa na lini kitalipwa.

(c) Je, ni ipi sababu ya Serikali kuchelewesha malipo ya kazi hiyo na kwa mwaka wa fedha 2022/2023 deni hilo limekusudiwa kulipwa kwa programu ipi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

7. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Hatuna budi kuishukuru Serikali yetu kupitia Wizara hii kwa juhudi inazozichukuwa katika kuinua michezo na afya za vijana wetu hapa nchini, ikiwa ni pamoja na kuwapatia viwanja bora vya michezo ya mpira.

Je, ni lini Wizara yako itafikiria kukikarabati kiwanja kimoja wapo cha mchezo wa mpira wa miguu katika jimbo la Mwanakwerekwe.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

28. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Wananchi wa Zanzibar wana matumaini makubwa sana ya kujikwamua kiuchumi kupitia Sera ya Uchumi wa Buluu katika

kilimo cha mwani hususan katika jimbo la Tumbe ambalo hutoa kiwango bora na kikubwa cha mwani kila siku.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuwajengea makaushio wakulima hawa ili kuwarahisishia kazi zao.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

36. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Serikali imekuwa ikifanya kila juhudi kuhakikisha utalii wa Zanzibar unakuwa ni kivutio kikubwa cha dunia kutokana na mambo mbali mbali ya kuvutia kama vile fukwe za bahari, bidhaa za viungo vyenye harufu ya kipekee, sanaa na ukarimu wa wananchi wake. Hata hivyo, katika kuuenzi utalii huo kumekuwa na uzorotaji wa mikakati ambayo itapelekea Zanzibar kujulikana zaidi kwenye sekta hiyo.

(a) Je, Serikali itatumia njia gani za kuitisha Utalii wa Mikutano ya Kimataifa (Tourism Conferences), ili kusaidia kuutangaza utalii wa Zanzibar duniani.

(b) Serikali inauangalia vipi Utalii wa Mikutano ya Kimataifa (Tourism Conferences), kufanyika katika mahoteli na maeneo mbali mbali ya vivutio vya utalii hapa Zanzibar.

**Wizara ya Afya:**

92. MHESHIMIWA SABIHA FILFIL THANI (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunawapongeza viongozi na wananchi wa Ndijani Mseweni kwa kujenga kituo cha Afya kwa nguvu zao na Serikali kuunga mkono kwa kumalizia ujenzi wa kituo hicho.

Kwa vile kituo hicho ni cha muda mrefu na kimekuwa chakavu sana, Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo kipya au kukifanyia matengenezo kituo hicho.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

6. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ukulima wa asali bado haujazingatiwa kama vinavyozingatiwa vilimo vyengine vya mazao ya kawaida, hali inayoaminika, pamoja na sababu nyengine, bado Serikali yetu haijachukua juhudi ya kutosha kuwaelimisha wananchi wetu juu ya faida inayopatikana kutokana na kilimo cha asali.

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali yetu imekuwa inawasaidia wajasiriamali wanaojishughulisha na ufugaji wa nyuki hapa nchini.

(b) Je, Serikali imetoa kwa kiasi gani elimu kwa wananchi wetu kuwa asali ni zao litakalowawezesha kujikwamua na umasikini.

121. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Suala la hewa ukaa lilitawala sana katika nyoyo za watu wetu, jambo ambalo liliwapa hamasa ya kuongeza bidii kubwa ya upandaji wa mikoko zaidi kwa lengo la kujipatia kipato.

(a) Je, suala la kuhamasisha wananchi kupanda mikoko hadi sasa limefikia wapi.

(b) Ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi wetu juu ya kupanda mikoko.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

34. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar:

Tunaipongeza sana Serikali kwa kuiimarisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST) katika nyanja mbali mbali, ikiwa

ni pamoja na kuijengea uwezo ili hatimae iweze kujitegemea. Hata hivyo, imebainika kwamba, wanafunzi waliosajiliwa kujiunga na masomo katika Taasisi hiyo kwa mwaka wa masomo 2022/23, katika ngazi tofauti, kutozwa fedha takriban Shilingi za Kitanzania Elfu Sitini (Tsh. 60,000/) kwa ajili ya usafiri hata kama wanafunzi hao hawahitaji usafiri wa Taasisi hiyo.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri kwa kiasi gani unalifahamu suala hili, linaloendelea kufanyika katika Taasisi hiyo.

(b) Je, ni kanuni au kifungu gani cha sheria ya Taasisi hiyo kinachotoa fursa kwa uongozi wa Taasisi hii kufikia maamuzi hayo.

(c) Je, huoni kuwa kitendo cha kuwatoza wanafunzi hao kiwango hicho cha fedha hakiwatendei haki wanafunzi hao na hasa ikizingatiwa kuwa hali zao za uchumi ni duni.

88. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Maeneo mengi ya majengo ya Serikali yakiwemo mashule hayana hati miliki, jambo ambalo linapelekea kuvamiwa kwa ujenzi wa makaazi ya wananchi.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuyapatia hati miliki maeneo hayo.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

18. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na kujenga miradi mbali mbali ya maji katika Jiji la Zanzibar ikiwa ni pamoja na mradi mkubwa wa maji uliopo Kwarara, Wizara yako imekuwa inakabiliwa na changamoto kubwa ya baadhi ya miradi ya maji inayoisimamia kutoleta tija iliyokusudiwa.

(a) Je, kuna sababu zipi za msingi zinazoipelekea changamoto hiyo kujitokeza mara kwa mara katika Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA).

(b) Je, ni lini viogozi wa Wizara yako, ukiwa ni pamoja na wewe Mheshimiwa Waziri, mtafanya ziara kuja kusikiliza na kuzipatia ufumbuzi baadhi ya kero za maji katika maeneo mbali mbali jimboni Mwanakwerekwe.

(c) Je, Mamlaka ya Maji ya Zanzibar (ZAWA) iko tayari kusaidia wataalamu watakaowaelekeza wananchi wa jimbo la Mwanakwerekwe maeneo sahihi na muafaka kiafya ya kuchimba visima.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

110. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa kipindi kirefu Serikali yetu inachukua juhudi mbali mbali ili kuhakikisha inaimarisha bei za bidhaa zinazozalishwa na wakulima wetu wa ndani hapa Tanzania, dhidi ya bidhaa zinazotoka nje ya nchi ambazo huathiri upatikanaji wa soko la bidhaa zinazozalishwa nchini.

(a) Kwanini bidhaa ya mchele wa Mbeya unaozalishwa ndani ya Tanzania una bei kubwa ukilinganisha na mchele wa mapembe unaotoka nje ya nchi.

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha bei ya bidhaa hiyo inakuwa ndogo, ikilinganishwa na bei za bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:**

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti bora ndani yake.

**Zanzibar,**
**13 Disemba, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**